

FASIHI YA WOTOTO KATIKA KUTEKELEZA MAHITAJI YA MTOTO KISAIKOLOJIA

Pamela M.Y. Ngugi

Ikisiri

Lengo la makala haya ni kubainisha umuhimu wa fasihi ya watoto katika kutekeleza mahitaji yao kisaikolojia. Katika kufanya hivi tumezingatia masuala mbalimbali yanayohusu sifa bainifu za watoto pamoja na kujadili vipengele muhimu katika fasihi ya watoto na kuonesha jinsi vinavyochangia katika kumnufaisha mtoto kisaikolojia.

1.0 Utangulizi

Kila mwandishi huwa na sababu zake mbalimbali au hata mtazamo, itikadi, falsafa pamoja na mwelekeo wake binafsi kuhusu majukumu ya fasihi kwa jamii (Wamitila, 2008), na vilevile kuhusu wajibu wake kama mwandishi kwa jamii anayoiandikia. Hivyo basi, kila kazi ya fasihi huwa na jukumu maalumu la kisaikolojia kwa wasomaji lengwa (Sanders, 1967). Kwa mfano, Sanders (1967) anamnukuu mwanafasihi maalum, James Baldwin aliyehoji kuwa jukumu la mwandishi ni kueleza mambo ambayo watu wengine hawana nafasi ya kuyaeleza. Kwa sababu hiyo huenda mwandishi kama huyo ataibua fasihi iliyo na mtazamo wa kisaikolojia ambao ni tofauti na ule aliopendekeza Emily Dickinson aliyehoji kuwa, “Hakuna chombo chochote kama kitabu kinachoweza kutupeleka katika nchi za mbali.” Au hata maoni aliyotoa Toltoi kuwa, “Usanii ni kitendo cha binadamu kilicho na jukumu la kupasha hisia za kindani kwa watu wengine”. Mitazamo hii kuhusu fasihi kwa jumla inadhihirika pia katika fasihi ya watoto. Swali ni, je, kati ya majukumu haya ya fasihi, ni yapi yaliyo muhimu zaidi kwa watoto? Katika makala haya tutajaribu kuonesha namna fasihi ya watoto inavyowafaidisha watoto kisaikolojia. Kwanza, kwa kubainisha mahitaji ya kisaikolojia ya watoto. Pili, kuonesha nafasi ya fasihi ya watoto na namna inavyochangia katika kumkuza mtoto kisaikolojia na mwisho tueleza vipengele vya kimsingi vinavyochangia motisha ya kusoma miongoni mwa watoto.

1.1 Mahitaji ya Kisaikolojia ya Watoto

Ili kubainisha haya, itatubidi kujibu maswali kadha wa kadha kuhusiana na mahitaji ya watoto wanapoendelea kukua. Swali la kwanza ni, Je, ni sifa zipi maalumu zinazodhihirika katika maisha ya mtoto? Ukweli ni kwamba watoto bado wanaendelea kukua kimwili, kisaikolojia na wanategemea watu wazima kuwaelekeza. Katika kukua kwa mtoto yeye hujaribu kuuelewa ulimwengu wa nje anamokulia na unaopanuka kila kukicha na vilevile anajaribu kuuelewa ulimwengu

wake wa ndani hasa kwa hujaribu kuelewa hisia zake ambazo huwa hazijaimarika moja kwa moja bali huyumbayumba.

Katika hali hizi mbili, kuna tajiriba nyingi zinazohitaji kueleweka. Kwa mfano, mtoto angetaka kujua ni kwa nini mvua hunyeshwa? Au hata 'ni kwa nini binadamu hulua? Mtoto anapoelewa maswali kama haya, huwa anaanza kupata nguvu za aina fulani. Kuna matakwa ya kilimwengu ambayo mtoto anahitaji kujifunza na kuyatekeleza kuanzia kwa kuwa na misimamo yake hadi kuipokea au kuikataa misimamo ya makundi rika. Vilevile kuna matakwa ya ndani ambayo mtoto anahitaji kuyatekeleza. Kwa mfano, kujua namna ya kudhibiti hasira zake na namna ya kukabiliana na njaa. Ama akiweza kukabiliana na matakwa haya kwa njia maalumu basi itachukuliwa kuwa anaanza kuelewa ulimwengu wake wa ndani na nje. Fasihi inaweza kuchangia katika kumsaidia mtoto kukubali hali fulani na hata kujua namna ya kukabiliana na hali nyinginezo ambazo zitaendelea kuibuka katika maisha yake kila kukicha.

Wanasaikolojia wengi wanakubaliana kuwa kuelewa mahitaji ya kimsingi ya watoto ni hatua muhimu katika kufanikisha masomo yake. Kwa mfano Salehi (2011) anahoji kuwa watoto wote huwa na mahitaji ya kisaikolojia; na kwamba hisia za watoto huwa dhaifu kiasi kwamba mahitaji haya yakipuuzwa basi watoto wataweza kukabiliana na matatizo mengi katika siku za mbeleni. Hivyo basi, ili kupata mafanikio katika maisha ya mtoto ya baadaye, ni muhimu kutambua mahitaji yao ya kimsingi, pawe na jitihada za kusuluhisha matatizo fulani wanayokumbana nayo na suluhu zinazotolewa zinahitaji kuwa zenye mantiki na zilizosawazishwa. Watoto huwa na mahitaji tofauti na hudhihirisha kuwa wanawategemea wazazi kupitia mahitaji haya. Mahitaji ya kimsingi kwa watoto ni: lishe bora, kutaka kuzingatiwa na kuishi katika hali ya usalama. Mbali na mahitaji haya ya kimwili, watoto huwa na hitaji la kudadisi na kutekeleza udadisi huo. Wao hutaka kudadisi mazingira yao kiuhalisi na kisaikolojia. Kwa sababu hiyo ni muhimu kufikiria kuhusu mada zinazofaa kwa kila mtoto katika vitabu vya watoto na vijana. Jambo hili litachangia katika kutimiza hamu yao ya udadisi.

Katika kuchunguza ukuaji wa watoto, wanasaikolojia wametambua viwango mbalimbali vya ukuaji miongoni mwa watoto. Kwa mfano, mtaalamu Piaget (1958) amesainisha viwango vya utambuzi katika maisha ya mtoto ambavyo ni: kiwango cha Mienendo Hisia (*Stage of Sensory – Dynamic*), Hatua kabla ya kazi (*Pre-operational stage*), kiwango cha Awamu ya Utendaji (*Pre-Operational stage*), na mwisho ni kiwango cha Awamu ya shughuli Rasmi (*Stage of Formal Operations*). Hatutajadili viwango hivi lakini muhimu ni kutaja kuwa kuna vifaa maalumu vya kibaiolojia anavyoleta mtu katika ulimwengu anapozaliwa. Vifaa hivi hujengwa na kukuzwa kwa kutegemea tajiriba ya ukuaji wa kila kipindi cha ukuaji katika maisha

ya mtoto. Baadhi ya tajiriba hizi ni za kijumla lakini zingine zinategemea kila mtoto kwa upekee wake.

1.2 Nafasi ya Fasihi katika kutimiza Mahitaji ya Kisaikolojia ya Mtoto

Inaeleweka kuwa maendeleo makubwa ambayo yametekelezwa na binadamu ni kuibua fasihi ulimwenguni. Ugunduzi huu unawakilisha kiwango cha juu cha mafanikio ya binadamu. Kupitia chombo hiki, ugunduzi wa kitu fulani uliofanywa na mtu mmoja unaweza kupokelewa na watu wengine walio mbali zaidi kimaeneo na hata katika kizazi kimoja hadi kingine. Baadhi ya watoto wameweza kutambua hili, na wanatarajia fasihi kutoa mafunzo yaliyo muhimu kwao. Kauli hii iliwahi kutolewa na mwanafasihi Rosenblat (1995). Rosenblatt (Keshatajwa), anaamini kwamba usomaji ni mapatano ambayo hudhihirika kwa njia mbili kuu. Njia ya kwanza inahusu ujumi ambao hujumuisha kufikiria, kuhisi na kupata tajiriba kutokana na kusoma fasihi. Njia ya pili inahusu kile anachokiita, '*effeferent*' ambayo inarejelea ile hali ya kupata taarifa kupitia usomaji wa vitabu mbalimbali. Kwa njia hizo basi, kila msomaji hufanya mapatano yake kwa sababu tofauti. Hivyo basi, watoto wanahitaji kupewa nafasi ya kusoma vitabu vingi na vya aina mbalimbali kulingana na yale mapatano wanayoyafanya katika usomaji wao.

Hata hivyo, jambo hili huenda lisijitokeze moja kwa moja kwa sababu huenda watoto wengine wakawa na matarajio hasi kuhusu hadithi fulani waliyoisoma. Muhimu ni kwamba hata ikiwa matarajio ya msomaji ni hasi au chanya, ujumbe fulani unahitaji kupashwa kwa msomaji. Iwapo mtoto atahisi kuwa kile anachokisoma ni muhimu kwake, na kwamba kutokana na usomaji huo ataweza kupata mbinu fulani ya kutekeleza jambo analotaka kutimiza, au atajua ukweli fulani au akaelewa hisia fulani ambazo zimekuwa zikimsumbua, basi ina maana kuwa ujumbe umepokelewa, mtoto anaweza kupata funzo fulani kutoka kwenye hadithi aliyoisoma.

Ili kuhakikisha kuwa mtoto amepata tajiriba ya kifasihi kama chombo muhimu kisaikolojia, basi vitabu anavyovisoma katika awamu ya mwanzo maishani huwa muhimu (Huck, 1979). Ni kweli kwamba kwa muda mrefu kipengele hiki kimepuuzwa na wadau wanaosimamia miradi ya usomaji kwa wototo. Kile kinachobainika ni usomaji wa juu juu ambao mara nyingi haujali sana yaliyomo. Kwa bahati nzuri mtazamo huu umeanza kubadilika kutokana na baadhi ya wadau kuchukulia mradi wa usomaji kwa dhati na kuziba pengo hili. Tatatizo linaloibuka tunaposisitiza sana usomaji usio makini ni kwamba umuhimu wa kijamii na kisaikolojia wa usomaji unatupiliwa mbali.

Fasihi inaweza kuwasaidia watoto walio na matatizo ya kusoma hasa yale yanayohusu uwezo wa kutambua herufi fulani fulani (Sanders, 1967). Watoto kama hawa wanaweza kufunzwa namna ya kukabiliana na hali hii kwa kupewa vitabu

mbalimbali vya fasihi. Kupitia vitabu hivi, wataweza kung'amua aina mbalimbali za herufi zinapowekwa kwa pamoja na kuelekezwa kusoma herufi hizo kwa pamoja. Mtoto kama huyu anapojua kuwa amepiga hatua na kufanikiwa katika usomaji, basi jambo hili linampa motisha ya kutaka kusoma zaidi na hivyo anaridhika kisaikolojia.

Kimsingi ni kwamba ili mtoto aweze kufaidika kutokana na kile anachokisoma, ujumbe wa hadithi hiyo unahitaji kumhusu mtoto huyo. Akifanya hivi atakuwa anasoma kile ambacho kinaweza kumsaidia katika maisha yake: iwapo ni kudhibiti hisia mbalimbali, kubadilisha mienendo fulani au hata kupata maarifa fulani ya kumsaidia maishani.

Namna mada fulani inavyoshughulikiwa, na kule inakoelekezwa ni muhimu. Kwa mfano, baadhi ya hadithi ambazo zimesilimishwa kutoka katika Biblia zinawavutia watoto kwa sababu zinahusu ushahi mwingi na mambo mengine maovu anayoyatenda binadamu. Hadithi hizo pia huonesha namna hali kama hizo zilivyokabiliwa na wanajamii. Tunaona kuwa baadhi ya hatua zilizochukuliwa kwa watendaji wa vitendo hivyo ni kali mno. Kwa mfano, tunaona kuwa uwasilishaji wa hisia za wivu miongoni mwa marika kama ilivyofanyika kwa Kaini na Abeli (Biblia: Habari Njema, 1972: Mwanzo 4), na hatua zilizochukuliwa kwa Kaini ni namna moja ya kuwatahadharisha watoto kuhusu umuhimu wa kudhibiti hisia za wivu. Hadithi kama hizi ambazo hutolewa kwa njia iliyosahili na kwa njia ya moja kwa moja huwa zinaeleza mambo ya kimsingi maishani na namna ya kukabiliana nayo.

1.3 Vipengele vya Kimsingi katika Fasihi ya Watoto

Katika kufikiria kuhusu fasihi ya watoto, jambo muhimu tunalohitaji kujiuliza ni je, mada inayozungumzwa ni mada inayoweza kuwavutia watoto? Pili, je, mada hiyo imewasilishwa kwa njia ambayo mtoto anaweza kuikubali na vilevile iwe na maana kwa tajiriba yake? Maswali haya yanaweza kujibiwa kwa kuzingatia kanuni za kimsingi zinazohusu ukuaji wa watoto kisaikolojia zilizopendekezwa na Salehi (2011). Kanuni hizi ni pamoja na:

1.3.1 Ujengaji wa Shauku

Kuwa na shauku katika kujua au kutenda jambo fulani ni miongoni mwa mahitaji ya kimsingi ambayo yanachangia ufanisi wa kufunzwa na kujifunza. Iwapo mtoto hana shauku katika somo fulani basi hataweka makini katika somo hilo. Ukweli ni kwamba watoto huwa na shauku kubwa katika mazingira yao hasa kuhusu wanyama, ndege na vitu vingine. Hivyo basi, katika kutunga vitabu vya watoto ni muhimu kuzingatia shauku mbalimbali za watoto. Tusipozingatia shauku

mbalimbali za watoto tutaishia katika kudidimiza au kuuu shauku zao na hivyo basi kuvunja motisha ya kusoma.

1.3.2 Kuelewa Makundi mbalimbali ya Watoto

Kanuni hii inahusu mwandishi kuelewa watoto katika viwango mbalimbali vya umri. Kanuni hii inahitaji wandishi kuzingatia kiwango cha uelewa cha kila mtoto. Hii inatokana na ukweli kuwa mada zilizo ngumu na tata zinaweza kumchosha msomaji asiyemakinika katika harakati ya usomaji. Ni muhimu kuzingatia usahili katika uwasilishaji. Isitoshe, tunahitaji kuwapa watoto vitabu ambavyo vinashughulikia mada mbalimbali na visilimishwe kwa kuzingatia talanta zao. Vile vile, kile wanachosoma kinahitaji kulandana na maarifa ya awali waliyonayo. Muhimu ni kujua kwamba ili kujenga mielekeo chanya kuhusu vitabu, vitabu vinavyoandikwa na kuteuliwa kwa minajili ya kusomwa na watoto vinahitaji kulingana na umri na uwezo wao wa kiakili (Ngugi, 2011).

Hata hivyo, tunaposhughulikia watoto huwa kuna mtindo hatari wa kutaka kusahilisha mambo kupita kiasi na wakati mwingine kuepuka kushughulikia maeneo ambayo yanaonekana tata na magumu na ambayo hayataleta furaha kwa mtoto. Hali hii hutokana na kule kusisitiza kupita kiasi kwamba watoto wangali wachanga na vilevile hawana uwezo wa kiakili wa kuyapokea mambo magumu badala ya kuangalia kuwa wanaendelea kukua na kupanua uwezo wao wa kuelewa mambo tata (1989). Hali kama hii inaweza kupinga umuhimu wa fasihi kwa watoto, kwa sababu itaelekeza katika kuondoa yale mambo ambayo ni muhimu sana kwa mtoto kupitia kwa fasihi. Yapo mambo katika maisha ambayo yakipuuzwa sana, hayataeleweka na mtoto baadaye; na yakielezwa kwa njia iliyo sahili kupita kiasi, hayatamsaidia mtoto. Ili kuhakikisha kuwa mtoto anafaidika, mambo haya yanahitaji kuwasilishwa kwa njia ambayo inamsaidia mtoto kujua namna ya kukabiliana na hali kama hizo. Sanders (1967) anadai kuwa jinsi tunavyowachukulia watoto ndivyo watoto hawa wanavyojichukulia. Anasisitiza kuwa iwapo watoto wanapewa heshima basi hata wao watajiheshimu katika matendo yao. Lakini iwapo tutawapa mkebe kutumia kama kikombe kwa sababu tunafikiria kuwa hawajali au watawunja kikombe cha kauri basi hata wao hawatajali lakini iwapo watapeleka kikombe cha kauri ili waone umaridadi uliomo katika kikombe hicho, basi wataweza kukiheshimu kikombe hicho. Hii ina maana kuwa iwapo tutawapa fasihi ambayo inawapa uwezo wa kufikiri basi hata wao wataanza kudhihirisha tabia za werevu.

1.3.3 Umuhimu wa fasihi

Ili mtoto aweze kunufaika kutokana na kitabu fulani ni muhimu kuona kuwa kile kinachozungumziwa kina umuhimu kwake. Iwapo tutazingatia ukuaji wa watoto pamoja na shauku zao, tutagundua kuwa kuna mada fulani ambazo huonekana muhimu kwa kila mtoto katika kila kipindi cha maisha yake. Ujumbe wa hadithi

hiyo unahitaji kumhusu yeye mwenyewe. Akipata kile kilicho muhimu kwake basi kitamsaidia katika maisha yake. Kwa mfano, iwapo mtoto aliye na matatizo ya kudhibiti hisia zake mbalimbali, kubadilisha mienendo fulani au hata kupata maarifa fulani, akipata kitabu ambacho kitalenga mambo haya kitaweza kumfaa mtoto huyu zaidi. Kupitia kudhibiti hisia zake mtoto atakuwa anajenga uhusiano mwema na watu wengine na vile vile akawa anajitambua yeye mwenyewe na hulka yake. Hii ndiyo sababu Ngugi (2011) alipendekeza umuhimu wa wadau kama vile walimu na wazazi kutambua hulka mbalimbali za watoto ndiposa waweze kuwachagua vitabu ambavyo vitawafaa.

1.3.4 Uhalali na Ukweli katika Fasihi

Kanuni nyingine na ambayo ni muhimu katika vitabu vya watoto ni uwasilishaji wa mambo kihalali. Ujumbe unaopatikana katika kitabu fulani huwa ni halali iwapo ni wa kuaminika na wa kweli. Kwa mfano, Sanders (1967) anakiri kuwa ujumbe unaotolewa kwa watoto kuhusu kitendo cha kujamiiana huwa si kweli au hata hakuna ujumbe kama huo unaopokezwa kwa watoto. Sanders (keshatajwa) anadai kuwa kwa kweli watoto hawana shughuli na mambo haya ya watu wazima ila wana mvuto kwa miili yao wenyewe ikiwemo sehemu zao za siri, mapenzi miongoni mwa watu wazima na hata suala la kujamiiana, lakini haya yote ni kwa mtazamo wao wa kitoto. Tunapouficha ujumbe huu au kuupuuza, mtoto huchukulia kwamba watu wazima hawataki watoto wayajue mambo haya ya kujamiiana kwa sababu hata vitabu haviandikwi vikigusia mambo haya.

Kuna tatizo katika usahilishaji wa kupita kiasi wa taarifa fulani zinazotolewa kwa watoto. Kwa mfano, ni wazi kwamba wazazi hutoa maelezo tofauti kuhusu kitendo cha kushika mimba. Taarifa kama hizi huwakanganya watoto wengi. Mara nyingi watoto huelezwa kuwa mbegu ya baba na yai la mama hukutana na hapo mtoto hupatikana. Tatizo ni kwamba kwa mtoto mdogo, taswira inayomjia ni ile ya mbegu kama ya mboga na yai la kuku ambalo amezoea kuliona katika mazingira yake. Katika muktadha kama huu tunaona kuwa usahilishaji wa kupita kiasi umepotosha ujumbe. Sanders (keshatajwa) anapendekeza kuwa ni muhimu kutumia neno mwafaka tunapowafunza watoto kwa sababu neno hilo ingawa ni la kisayansi na gumu kueleweka halitazua picha potofu. Vilevile neno hilo halitatatiza uelewa wa mtoto wakati mtoto huyu atakapokua kihisia na kiakili kiasi cha kuanza kuelewa mambo.

Hadithi nyingi za kimasimulizi hubeba ukweli ndani mwake. Kwa mfano, hadithi za Kihistoria, hadithi za kiuhalisia na hata masimulizi ya kisayansi. Hadithi kama hizi huakisi amali muhimu katika ukuaji wa mtoto. Amali hizi kama anavyosema Akoleti (1990) hujumuisha mahitaji ya utotoni kama vile mapenzi, kushinda woga,

usalama, mafanikio miongoni mwa amali nyinginezo. Hadithi kama hizi zinaweza kumfaa mtoto kisaikolojia kwa kummulikia hali ya mambo jinsi yalivyokuwa au yalivyo sasa.

Sanders (1967) anasema kuwa fasihi inaweza kutazamwa kwa namna mbili tofauti: Ama inaweza kuchukuliwa kuwa fasihi inamtoa msomaji kutoka hali yake duni na kumpeleka katika ulimwengu wa raha mustarehe ambapo upande ule mwingine wa maisha ya binadamu yaliyojaa masaibu yanapuuzwa, au fasihi isipuuze pande zote za maisha ya binadamu au hata inaweza kupuuza ule upande wa maisha mazuri. Hata hivyo, Sanders (kashatajwa) anaona tatizo katika mitazamo hii yote. Anahoji kwamba iwapo upande wowote utawasilishwa kwa njia ya kupiga chuku, basi tutakuwa tunatoa picha potofu ya maisha. Na iwapo mtoto atachukulia pande hizi zote kuwa ni ukweli kwa kuona kuwa watu wote wana furaha na ni wakarimu au hata iwapo fasihi inawasawiri watu wote kama wajinga na wasioweza kudhibiti hasira zao basi utakuwa ni upotovu wa hali ya maisha.

Muhimu ni kwamba kila upande wa maisha hutekeleza majukumu fulani ya kisaikolojia kwa mtoto unapotolewa kwa njia inayostahili. Tunnel na Jacob (1977) wanadai kuwa fasihi ya watoto ambayo inawasilisha pande mbili za kitu ni nzuri kwa sababu huonesha mbinu na maarifa fulani ya kutumia maishani. Kilicho muhimu hapa ni kile ambacho mtoto anaamini kuwa ni picha kamili ya maisha ya binadamu.

Cass (1967) anapendekeza kuwa hadithi za watoto zinahitaji kuonesha hali ambayo wema unashinda uovu. Ni kweli kwamba watoto huvutiwa na hadithi ambazo wavulana, wasichana na wanyama watundu huadhibiwa kwa sababu ya vitendo viovu. Kawaida adhabu inayotolewa isiwe kali au yenye nia mbaya lakini iwe ya kadri ili mtoto apate hisia za kutosha kuwa haki imetendeka. Cass (keshatajwa) anapendekeza kuwa watoto wasinyimwe haki ya kuwa na masikitiko na uchungu hata kama ni kwa kiwango kidogo tu. Kushiriki katika masikitiko ya wengine ni kujihusisha na masikitiko ya binadamu huwafanya watoto waelewe ubia wa hisia za binadamu, kutoelewana, kukasirika na kupoteza matumaini (Ruthiiri, 2012).

1.3.5 Kanuni za Uwasilishaji wa Fasihi ya Watoto

Katika kuzingatia umuhimu wa fasihi kisaikolojia, tunahitaji kujiuliza swali kuhusu mbinu za uwasilishaji wa kazi za watoto. Je, mtoto anaelewa ujumbe uliowasilishwa? Kile kinachotofautisha fasihi ya watoto na ya watu wazima ni muundo, umbo na lugha inayopatikana katika kazi za watoto.

Jambo la kwanza linalosaidia kuleta mvuto kwa fasihi ya watoto ni umbo la kitabu (Ruthiiri, 2012). Mambo kama vile ukubwa, muundo na umbo, vielezo, taipografia,

ubora wa karatasi na ujaladishaji huwavutia watoto kwa vitabu. Picha na maandishi makubwa huwa muhimu kwa kiwango fulani cha watoto. Watoto wanapoona vitu walivyozoea kuviona katika mazingira yao huweza kuafikiana na hadithi hiyo. Vilevile, matumizi ya picha huwa muhimu hasa kwa watoto ambao uelewa wao wa mambo ni wa kiwango cha chini. Kwa mujibu wa Allen (1989), picha zinaweza kuonesha vitu muhimu ambavyo havikuwa vimetambulika na kueleweka hapo awali katika usomaji wa hadithi.

Cass (1987) anaongezea kwa kusema kuwa rangi inayotumiwa katika vitabu vya watoto inaweza kuwa na mvuto kwa usomaji wa kitabu fulani. Cass (keshatajwa) anahoji kuwa watoto huchagua vitabu vilivyo na mngaro wa hali ya juu. Kwa mfano, rangi nyekundu huwa na mvuto mkubwa kwa watoto ikifuatwa na rangi ya manjano, samawati na kijani kibichi.

Jambo jingine ni jalada la kitabu, ujalidi na anwani ya kitabu. Uhakiki wa kitabu cha watoto huanzia kwenye jalada. Jalada hubeba ujumbe kwa muhtasari wa hadithi iliyo ndani ya kitabu. Hivyo basi, ujumbe kwenye jalada unahitaji kuwa wenye mvuto. Katika fasihi ya watoto, vielelezo kwenye jalada huweza kuwa ndicho kigezo kinachompa mtoto motisha ya kusoma kitabu fulani. Ujalidi unahusu umbile la jalada na jinsi lilivyounganishwa na kurasa zingine. Ujalidi uliofanywa vizuri ni ule ulio imara ili kitabu kiweze kudumu kwa muda mrefu.

Pia, rangi iliyo kwenye jalada la kitabu cha watoto yapaswa kuwa angavu na ya kuvutia. Kiungo muhimu kabisa katika umbo la kitabu ni vielelezo au ule uwasilishaji wa maneno kwa kutumia picha. Katika fasihi ya watoto hasa watoto wa kiwango cha chini, vielelezo husadia sio tu kukifanya kitabu kivutie machoni mwa mtoto lakini pia husisitiza dhana muhimu katika kitabu. Aidha, vielelezo huwasaidia wasomaji ambao uelewa wao wa dhana ni wa kiwango cha chini (Benton na Fox, 1985; Ruthiri, 2012). Kimsingi ni kwamba vielelezo huwa na majukumu yafuatayo:

1. Hutoa kielelezo cha matini au hadithi;
2. Huleta mvuto kwa msomaji;
3. Hueleza kwa muhtasari wazo kuu;
4. Husaidia kuondoa uchovu wa msomaji;
5. Humsaidia mtoto kukumbuka hadithi, na
6. Hutoa ufafanuzi zaidi kuhusu sehemu ya hadithi.

Katika matumizi ya vielelezo, mwandishi na mchoraji wa vielelezo wanahitaji kuhakikisha kuwa vielelezo vimewasilishwa kwa namna ambayo watoto wanaweza kuelewa kwa haraka. Vile vile, wahakikishe kuwa vielelezo hivyo vinaakisi vitendo

vya wahusika na vilevile vinaoana na ujumbe uliokusudiwa. Vielelezo vinavyotumika kwenye jalada ni muhimu sana na inafaa vichorwe kwa makini ili viingiliane na anwani ya kitabu na yaliyomo. Vielelezo mwafaka huwekwa kwenye ukurasa mmoja na matini inayowakilishwa au inayorejelewa. Hata hivyo, Smith na wenzake (1970) wanaona kuwa sio lazima mwandishi na mchoraji watumie vielelezo hasa pale ambapo anahisi kuwa watoto wataweza kuisoma na kuelewa matini isiyoshirikisha vielelezo.

Taipografia au maneno pia huwa muhimu. Katika vitabu vya watoto taipografia inapaswa kuwa kubwa kulingana na kiwango cha watoto. Herufi ndogo ndogo mara nyingi hazivavutii watoto hasa wanapolazimika kukaza macho wanaposoma (Hunt, 1994). Karatasi inayotumiwa inahitaji kuwa ngumu ili isiraruke kwa urahisi. Kipengele kingine cha kuzingatia ni urefu wa hadithi. Aghalabu, watoto huvutiwa na vitabu ambavyo watavisoma na kukamilisha katika kikao kimoja bila kukatisha usomaji wao. Hivyo basi, mwandishi anahitaji kutambua awali uwezo wa kuweka makini miongoni mwa watoto mbalimbali.

Ikiwa lugha iliyotumika ni ya kiwango cha juu sana, mtoto hataelewa, na ujumbe hautamfikia. Mwandishi wa vitabu vya watoto anahitaji kutumia lugha kwa ustadi na kwa kuzingatia kila kiwango cha wasomaji wake. Ni kupitia kwa lugha ndipo umaarufu wa mwandishi unakadiriwa. Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia kuwa, kwa kutegemea umri mbalimbali watoto huhitaji msamiati mpya ili kupanua uwezo wa kuwasiliana. Msamiati huu unahitaji kuambatana na kiwango chao cha utambuzi. Maneno yanayoteuliwa na waandishi wa vitabu pamoja na mpangilio wake yanaweza kufanya kazi yake ieleweke au isieleweke kwa watoto wa viwango tofauti. Pia, iwapo ujumbe umewasilishwa kwa njia ambayo inaibua hisia za dukuduku, basi mtoto hataweza kuafikiana na ujumbe huo. Namna ambavyo kazi fulani inawasilishwa ili kuibua dukuduku inahitaji kuhusiana sio tu na matokeo ya kisaikolojia bali pia jinsi ambavyo mwandishi huwasilisha ujumbe wake. Tatizo hutokea pale ambapo mwandishi anasawiri hali fulani ambayo inaibua dukuduku ya kiwango cha juu sana au hata dukuduku hilo halidhihiriki. Kwa mfano, hadithi za mazimwi ambazo huhusu vitisho vingi zaweza kuwasilishwa kwa njia ya kupiga chuku kiasi kwamba zinaendeleza woga badala ya kumsaidia mtoto kudhibiti hali kama hiyo.

Iwapo mada fulani ni muhimu kwa watoto lakini ni mada nyeti na tata hivi kwamba inazua dukuduku kwa watoto basi utanzu wa fantasia¹ unaweza kutumika kwa sababu matukio ambayo si ya kweli au yanayoonekana kuwa ya mbali zaidi

¹ Fantasia ni dhana inayotumiwa kuelezea kazi ya fasihi ambayo ina sifa ambazo zinakiuka hali halisi.

hayatakuwa na athari kubwa kwa hisia za mtoto kama yalivyo yale ya karibu sana na yanaweza kutendeka maishani. Kwa mfano, hadithi kuhusu Vita vya Trojani vinavyowasilishwa kifantasia ni rahisi kukubalika kwa mtoto bila kumtisha kuliko kuzungumzia mlipuko wa ugonjwa fulani katika jamii ya mtoto huyu; au hata kuzungumzia kuhusu vita vya kikabila katika jamii ambayo imeshuhudia vita kama hivyo. Hadithi inapowasilishwa kwa njia hii itamfikirisha msomaji kuhusu mambo anayoyaona katika ulimwengu halisi (Herman, 2012). Katika kufanya hivi mtoto, ataikubali hadithi hiyo na hapo hapo atajaribu kuangalia ulimwengu wake uliomzingira kwa jicho la upekuzi.

1.4 Hitimisho

Katika makala haya mambo muhimu yanayohusu fasihi ya watoto na jinsi inavyomfaa mtoto kisaikolojia yamejadiliwa. Jambo la kwanza limehusu kuelewa sifa za kimsingi katika ukuaji wa mtoto. Vile vile, ili kuhakikisha kwamba fasihi ina faidi kwa mtoto vigezo kama vile mahitaji ya kisaikolojia ya mtoto yamedokezwa pamoja na kuanisha vipengele vya kimsingi katika fasihi ya watoto. Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na ujengaji wa shauku, umuhimu wa kuelewa makundi mbalimbali ya watoto, suala la uhalali na ukweli katika fasihi ya watoto na kanuni za uwasilishaji wa kazi za watoto.

Marejeo

- Akoleit, J. (1990). "Response and Criticism in Children's Literature in Kenya: The Case of Barbar Kimenye," M.A Thesis, Kenyatta University.
- Allen, V.G. (1989). "Literature as Support to Language Acquisition." Katika Rigg, P. & V.G. Allen (wah) *When they don't Speak English: Intergrating the ESL into the regular Classroom*. National Council of Teachers of English. Urbana. 11-22
- Bee, H. (1989). *The Developing Child*. New York, Harper and Row Publishers.
- Benton, M. G. Fox (1985). *Teaching Literature: Nine to Fourteen*. New York. Oxford University Press.
- Chama cha Bibilia cha Kenya (1972) *Bibilia Habari Njema* . Chama cha Biblia cha Kenya, Nairobi.
- Cass, J. E. (1967). *Literature and the Young Child*. London: Longman Group Ltd.
- Herman, L. (2012). "Fantasia katika Fasihi ya Kiswahili kwa Watoto." Katika P.S. Malangwa & L.H. Bakize (wah) *Kioo Cha Lugha*. Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam. 122-134.
- Uck, C. na Wenzake. (2001). *Children's Literature in Elementary Schools* (toleo la 7). U.S.A. MCgraw-Hill Companies.

- Ngugi, P. (2011): *Language and Literacy Education: The State of Children's Literature in Kiswahili in Kenya*. Lambert Academic Publishing. Berlin.
- Piaget, J. (1932). *The Moral Judgement of a Child*. New York. Harcourt Brace.
- Rosenblatt, L. (1995). *Literature as Exploration*. New York. The Modern Language Association of America.
- Ruthiri, M.K. (2012). Tathmini ya Ufaafu wa Vitabu vya Kusoma kwa Madarasa ya 5 na 6 katika Shule za Msingi: Mifano ya Waandishi Wanne. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Salehi, A. (2011). "Foundations and Principles of Psychological Content of Children's Books." Makala yaliyowasilishwa katika Kongamano la Fasihi ya watoto. Bongokok. Psrcentre.org./ images/extraimages/36pdf. 27-2-2014.
- Sanders , J. (1967). "Psychological Significance of Children's Literature" Katika *The Library Quartely*. The University of Chicago Press. 15- 22. 27-2-2014.
- Smith na wenzake (1970). *Language and Thinking in Elementary Schools*. Rhinehart & Winston. New York.
- Tunnel, M.O. na Jacob, S. J. (1997). *Children's Literature Briefly*. U.S.A. Printice Hall International
- Wamitila, K.W. (2008). *Misingi ya Uchunguzi wa Fasihi*. Nairobi. Vide – Muwa Publishers Ltd.